

Jinsi ya kupata usafiri wa kwenda kwenye miadi yako ya chanjo ya COVID-19

Muhtasari

Ukiwa na Apple Health (Medicaid) na unahitaji usaidizi wa kupata miadi yako ya utunzaji wa afya, Health Care Authority (HCA, Mamlaka ya Utunzaji wa Afya) itagharamia usafiri wako. Unaweza kutumia huduma hii kwa miadi ya matibabu isiyo ya dharura kama chanjo za COVID-19

Jinsi ya kupata usaidizi wa usafiri

Piga simu kwa msaidizi wa usafiri wa kaunti yako (tazama orodha ya mawasiliano ya msaidizi kwenye ukurasa wa 2). Msaidizi huyo ataangalia ustahiki wako na kupanga usafiri unaotimiza mahitaji yako. Iwapo hustahiki kupata huduma hii, msaidizi atakuelekeza kwa rasilimali nyingine za ndani.

Tafadhali weka tayari taarifa ifuatayo unapopiga simu:

- Kadi yako ya huduma ya ProviderOne
- Anwani yako kamili ya uchukuaji
- Eneo la miadi yako ya chanjo
- Jina na nambari ya simu ya mhudumu wako wa afya (huhitaji taarifa hii ikiwa unahitaji usafiri wa kwenda kwa kituo cha chanjo ya COVID-19 ya cha umati)
- Tarehe na saa yako kamili ya miadi
- Aina ya miadi ya utunzaji wa afya (mfano, kuondolewa uchafu kwa damu, OB, meno, chanjo ya COVID-19, n.k.)

MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA

Usafiri kwa ajili ya matibabu yasiyo ya dharura ni nini?

Hii ni huduma ya kukusaidia kufika kituoni na kurudi nyumbani kutoka kwa miadi yako ya huduma ya afya. Aina za kawaida zaidi za usaidizi wa usafiri zinajumuisha basi yay umma, teksi, gari la kiti cha magurudumu, vocha za gesi, na kurejeshewa pesa ulizotumia kwa usafiri. Huduma hii haijumuishi machela, ambulensi, au usafiri wenye usalama.

Je, naweza kutumia usafiri wa matibabu yasiyo ya dharura kwa miadi ya chanjo ya COVID-19?

Ndiyo, tunagharamia usafiri wa kwenda na kurudi katika kituo cha afya ikijumuisha famasia, kliniki cha chanjo kwa umati, na kliniki za kuendesha kwenda. Tafadhali piga simu kwa msaidizi wa usafiri katika kaunti yako. Watapanga ziara inayotimiza mahitaji yako ya usafiri.

Ni nani anaweza kutumia usafiri kwa ajili ya matibabu yasiyo ya dharura?

Wateja wa Apple Health (Medicaid) wanaohitaji usaidizi wa usafiri wanastahiki kupata huduma hii.



Nafaa kupigia nani simu nikihitaji usafiri wa matibabu yasiyo ya dharura?

Wasiliana na msaidizi wa usafiri anayehudumia kaunti yako. Wataangalia ustahiki wako na kupanga ziara zako. Iwapo hustahiki kupata huduma hii, watakuunganisha na rasilimali nyingine za ndani.

Nafaa kupiga simu ili kuomba usafiri wakati gani?

Unafaa kupiga simu mara tu unapoweza, angalau siku mbili za biashara kabla ya miadi yako ya matibabu. Ziara za dharura zenye notisi ya chini ya siku mbili za biashara zinawezekana ikiwa rasilimali zinapatikana.

Njia za mawasiliano za msaidizi

Jina la msaidizi	Kaunti anazohudumia	Nambari ya simu
Hopelink	King, Snohomish	1-800-923-7433
Northwest Regional Council	Island, San Juan, Skagit, Whatcom	1-800-860-6812
Paratransit Services	Clallam, Grays Harbor, Jefferson, Kitsap, Lewis, Mason, Pacific, Pierce, Thurston	1-800-846-5438
Human Services Council	Clark, Cowlitz, Klickitat, Skamania, Wahkiakum	1-800-752-9422 (chaguo 2)
People for People	Benton, Chelan, Columbia, Douglas, Franklin, Kittitas, Okanogan, Walla Walla, Yakima	1-800-233-1624
Special Mobility Services	Adams, Asotin, Ferry, Garfield, Grant, Lincoln, Pend Oreille, Spokane, Stevens, Whitman	1-800-892-4817

Ili kupata maelezo zaidi, tafadhali nenda kwenye tovuti ya Non-Emergency Medical Transportation (NEMT, Usafiri wa Matibabu Yasiyo ya Dharura) kupitia hca.wa.gov/transportation-help.



820-NonDOH May 2021 Swahili

Ili kuomba waraka huu katika muundo mwingine, piga simu 1-800-525-0127. Wateja ambao ni viziwi au wasio na uwezo wa kuzungumza, tafadhali piga simu 711 (Washington Relay) au tuma barua pepe civil.rights@doh.wa.gov.

